

HALMASHAURI YA MJI HANDENI

TAREHE: 17.01.2019

TANGAZO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Handeni anayatangazia Makampuni binafsi yenye uwezo na uzoefu kujitokeza na kuomba kazi ya URASIMISHAJI WA MAENEO YA MAKAZI katika Mji wa Handeni kwenye Mitaa ya:-

1. Vibaoni
2. Kwedisewa
3. Azimio
4. Bomani
5. Komsanga
6. Bagamoyo
7. Komoza
8. Mabanda

A. KAZI ZITAKAZOFANYIKA:

1. Kuitisha mikutano kwa ajili ya Kutoa elimu kwa wananchi juu ya faida za kupanga, kupima na kurasimisha Makazi pamoja na uchangiaji wa gharama za urasimishaji.
2. Kutambua mipaka ya maeneo ya wamiliki wa maeneo yanayopangwa.
3. Kukusanya takwimu za awali za uwandani (field) kwa ajili ya kuandaa michoro ya Mipango miji
4. Kuandaa michoro ya Mipango Miji itakayojumuisha ramani ya miundo mbinu yote na huduma nyingine za jamii na kuipitisha katika ngazi zote zinazohusika ili wananchi wapate uelewa.
5. Kufanya uhakiki wa awali kwa maeneo yaliyopimwa kabla ya kuweka alama (beacons).
6. Kufanya kazi ya upimaji wa viwanja na kuweka alama (beacons).
7. Kupitisha ramani za upimaji katika mikutano ya wananchi kabla ya kuziwasilisha Wizarani.
8. Kuwasilisha kwa wananchi ramani za upimaji na mpango wa urasimishaji ambapo vvote vitakabidhiwa katika Ofisi

ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji na nakala kuwekwa katika Ofisi ya kata husika.


B. MASHARTI KWA MWOMBAJI:

1. Kampuni binafsi iwe imesajiliwa kisheria chini ya sheria ya usajili wa Makampuni, sura ya 212 (ya 2002).
2. Kampuni binafsi iwe imesajiliwa na Bodi ya Usajili wa wataalamu wa Mipango Miji chini ya usajili wa wataalamu wa Mipango Miji Na. 7 ya Mwaka 2007.
3. Kampuni iwe na sifa, uwezo, utaalamu na uzoefu katika kazi za urasimishaji kwa kipindi kisichopungua Miaka Mitatu (3).
4. Kampuni iwe na namba ya mlipa kodi kwa jina la Kampuni au la Mkurugenzi Msimamizi.
5. Kampuni iwe na wataalamu na rekodi nzuri kutekeleza kazi za urasimishaji.
6. Kampuni iwe tayari kufanya kazi na wananchi katika Mitaa na Kata itakayopangiwa.
7. Kampuni iwe na vifaa bora vya kufanyia kazi kama vile RTKGPS na vingine pamoja na usafiri wa uhakika wa kuweza kufika katika maeneo yote ya wananchi.

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P. 51,
HANDENI.

Limetolewa na:


.....

Kenneth K. Haule
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
HANDENI

